TANGAZO LA SERIKALI NA. 425 la tarehe 31/5/2024

SHERIA YA TOZO ZA BARABARA NA MAFUTA
(SURA YA 220)

# AMRI

*(Imetolewa chini ya kifungu cha 8(2))*

AMRI YA MSAMAHA WA TOZO ZA BARABARA NA MAFUTA KATIKA MRADI WA UJENZI WA MTANDAO WA MAJI KATIKA MIJI YA KAYANGA, CHATO NA GEITA UNAOTEKELEZWA NA WIZARA YA MAJI KUPITIA KAMPUNI YA AFCONS INFRASTRUCTURES LTD AND VIJETA PROJETS AND INFRACTRUCTURES LTD JV YA MWAKA 2024

Jina na kuanza kutumika

1. Amri hii itajulikana kama Amri ya Msamaha wa Tozo ya Barabara na Mafuta kwa mradi wa ujenzi wa mtandao wa maji katika miji ya Kayanga, Chato na Geita unaotekelezwa na Wizara ya Maji kupitia kampuni ya Afcons Infrastructures LTD and Vijeta Projets and Infractructures Ltd JV ya mwaka 2024.

Msamaha

2. Kwa kuzingatia masharti yaliyoainishwa katika aya ya 3 na masharti mengine yoyote kama yatakavyoainishwa na Kamishna Mkuu wa Mamlaka ya Mapato Tanzania, tozo zote za barabara na mafuta zinazopaswa kulipwa kwa mafuta yaliyoainishwa katika Jedwali la Amri hii yaliyoingizwa ndani ya nchi au kununuliwa kabla ya kibali kupitia forodha na Wizara ya Maji au kampuni ya Afcons Infrastructures and Vijeta Projets and Infractructures Ltd JV kwa niaba ya Wizara ya Maji kwenye mradi wa ujenzi wa mtandao wa maji katika miji ya Kayanga, Chato na Geita zinasamehewa.

Masharti

3. Msamaha uliotolewa chini ya Amri hii utakoma na tozo za barabara na mafuta zitapaswa kulipwa kana

kwamba Amri hii haijatolewa ikiwa mafuta yatatumika kwa matumizi mengine au yatahamishwa au kuuzwa kwa mtu mwingine ambaye hastahili kupata manufaa yanayotolewa na Amri hii.

Ukomo

4. Amri hii itafikia ukomo baada ya miezi kumi na mbili tangu tarehe ya kutangazwa katika Gazeti la Serikali.

---

JEDWALI

---

*(Limetengenezwa chini ya aya ya 2)*

| Na | Maelezo | Kipimo | Kiwango |
|---|---|---|---|
| 1. | Mafuta ya Taa | Lita | 100,000 |
| 2. | Mafuta ya transfoma | Lita | 50,000 |
| 3. | Mafuta ya Injini | Lita | 1,500,000 |
| 4. | Aina zote za vilainishi | Kg | 75,000 |
| 5. | Mafuta ya haidroli | Lita | 250,000 |
| 6. | Mafuta ya breki | Lita | 150,000 |
| 7. | Mafuta ya usukani | Lita | 150,000 |
| 8 | Mafuta ya Gia | Lita | 150,000 |
| 9 | Mafuta ya haidroli ya daraja 68/46/32 | Lita | 2,500,000 |

Dodoma,
13 Mei, 2024.

MWIGULU LAMECK NCHEMBA MADELU
*Waziri wa Fedha*